

# **HALMASHAURI YA WILAYA YA BUKOMBE**



## **TAARIFA FUPI YA WIKI YA CHANJO YA KITAIFA KUANZIA TAREHE 24 APRILI, 2017 HADI 30 APRILI, 2017**

Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe inaadhimishwa wiki ya chanjo kwa kuwashirikisha wazazi wote wilayani kwa kutoa chanjo kwa watoto wote wenye umri wa chini ya miaka mitano, ambapo Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto kupitia ujumbe wa wiki ya chanjo unaosema "chanjo hukinga kila mtu. "Pata chanjo" sambambamba na Kauli mbiu ya mwaka huu ni "Jamii iliyochanjwa ni Jamii yenyeye Afya"

Hivyo kupitia wiki hii ya chanjo ya kitaifa, vituo vyote vinavyotoa huduma za chanjo hapa Wilayani vitakuwa wazi kuanzia saa 2:00 Asubuhi hadi saa 11:00 jioni kila siku hadi tarehe 30 Aprili, 2017.

### **Chanjo zitakazotolewa ni kama ifuatavyo:**

1. Chanjo ya kuzuia kifua kikuu
2. Chanjo ya kuzua Pepopunda, Kifaduro, Dondakoo, Homa ya ini na Homa ya Uti wa Mgongo (chanjo hii inabeba chanjo zote tano kwa wakati mmoja).
3. Chanjo ya kuzuia kupooza
4. Chanjo ya kuzuia matumbo ya kuhara kwa watoto
5. Chanjo ya kuzuia kichomi (Pneumonia)
6. Chanjo ya kuzuia surua rubella (MR).
7. Chanjo ya Pepopunda (TT) inayotolewa kwa wanawake walio katika umri wa kuzaa ina lengo la kumkinga mtoto atakayezaliwa.

Chanjo hizi hutolewa kwa kufuata ratiba maalumu ya uchanjaji na kutolewa mara tu mtoto anapozaliwa kwa baadhi ya chanjo na hufuatiwa na chanjo kuanzia wiki ya sita, wiki ya kumi na wiki ya 14 tangu mtoto azaliwe, ataendelea kupata chanjo afikishapo miezi tisa na miezi 18. Baada ya

kupatiwa chanjo ya miezi tisa atapatiwa chandarua bila malipo. Ndipo tunaposema "**JAMII ILIYCHANJWA NI JAMII YENYE AFYA**".

Aidha tarehe 25 Aprili ya kila mwaka, huwa ni siku ya maadhimisho ya Malaria Duniani. Nasi leo tunaungana na Halmashauri nyingine nchini na Duniani kote kuadhimisha siku hii sambamba na wiki ya chanjo.

Tunatambua ugonjwa huu ni changamoto kubwa kwa wilaya yetu, na hivyo hatuna budi kukumbushana juu ya kujihami na kuudhibiti ugonjwa huu, na hivi leo tunatoa huduma ya upimaji na tiba ya malaria kwa watu wote bila malipo kabisa!!

### **HALI YA UTOAJI CHANJO HAPA WILAYANI**

Takwimu zinaonyesha kuwa tumekuwa tukifanya vizuri katika utoaji wa chanjo katika utaratibu wa kawaida na hata ule wa kampeni ya kitaifa.

**Kwa mfano mwaka 2016 kati ya watoto waliostahili kupata chanjo ni 10704 kwa mchanganuo ufuatao:-**

1. BCG walichanjwa watoto 10,524 sawa na 98%
2. POLIO 3 walichanjwa watoto 9,875 sawa na 93%
3. PENTA 3 walichanjwa watoto 9976 sawa na 93%
4. PCV 3 walichanjwa watoto 9,982 sawa na 93%
5. ROTA walichanjwa watoto 10,220 sawa na 95%
6. Surua rubella 1 walichanjwa watoto 9,548 sawa na 89%
7. Surua rubella 2 walichanjwa watoto 5,543 sawa na 53%

### **CHANGAMOTO:**

**Palipo na mafanikio changamoto hazikosekani**

- 1) Uchache wa vituo vya kutolea huduma za Afya na chanjo
- 2) Umbali wa maeneo hivyo kufanya wazazi na walezi washindwe kuwaleta watoto kupata chanjo kwa wakati

**3) Kuahirishwa kwa safari za chanjo kutokana na ukosefu wa magari usiotarajiwa.**

**NJIA AMBAZO ZIMEKUWA ZIKITUMIKA KATIKA KUPUNGUA  
CHANGAMOTO HIZI**

- 1) Kupeleka huduma za chanjo kwa njia ya mkoba na magari
- 2) Kuendelea kuhamasisha ujenzi wa vituo vyta kutolea huduma karibu na wananchi.
- 3) Kupanga tarehe nyingine za chanjo pale usafiri unapokosekana bila kutarajiwa.

Hotuba hii imewasilishwa na Dr.Irene Mukerebe Kaimu Mganga Mkuu wa Hospital ya Wilaya ya Bukombe.